# Uelekeo wa Maana za Kipolisemia katika Msamiati wa Kiswahili: Mifano kutoka Kamusi ya Kiswahili Sanifu

Faraja J. Mwendamseke

**Ikisiri**

Vipengele mbalimbali vya sarufi vinapopitia michakato ya mabadiliko vina uelekeo fulani. Pia, maana za maneno na tungo hukumbwa na mabadiliko mbalimbali. Mabadiliko ya maana za maneno huweza kutokea katika visawe na polisemia. Ullmann (1967) anaeleza kuwa polisemia ni sifa ya msingi katika mazungumzo ya binadamu ambapo licha ya kuwa na maana zaidi ya moja, maana hizo huwa zina uhusiano. Pia anaeleza kuwa kwa kiasi kikubwa polisemia hutokana na uhamishaji wa matumizi ya neno hilo kutegemeana na lugha inayohusika. Maelezo haya yanadokeza kuwa kuna uelekeo fulani wa mabadiliko ya maana katika polisemia. Katika makala hii tumechunguza uelekeo wa mabadiliko ya maana za kipolisemia katika lugha ya Kiswahili ili kueleza utokeaji wake na namna zinavyobainishwa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na changamoto zinazoweza kujitokeza katika ubainishaji huo. Data iliyotumika ni kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2013). Ili kukidhi malengo hayo tumetumia Nadharia ya Maana kama Dhana, ambapo tunahusisha maana (dhana) mpya za kipolisemia na maana ya msingi ya neno hilo. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa polisemia huwa na maana zaidi ya moja zinazohusishwa na fikra/wazo moja (maana ya msingi) na, utokeaji wake upo wa aina tofauti. Aina hizo; ni uhamishaji wa matumizi, ufananisho wa kisitiari, uwanja maalum katika jamii na kuwapo kwa maneno yenye asili ya kigeni. Kuna wakati utokeaji huu hutegemeana na aina ya neno husika kama ni nomino au kitenzi. Masuala haya hujibainisha wazi katika kamusi. Hata hivyo kuna baadhi ya changamoto zinajitokeza polisemia zinapobainishwa katika kamusi.

## 1.0 Utangulizi

Dhana ya polisemia imeelezwa na wataalamu mbalimbali. Baadhi ya wataalamu hao ni TUKI (2013) wanaofasili polisemia kuwa ni neno lenye maana mbili au zaidi zinazokaribiana sana kama vile "kupe" kwa maana ya mdudu na kupe kwa maana ya mtu anayeishi kwa kutegemea wengine. Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa polisemia ni uhusiano ambapo maana moja hutokana na maana ya neno jingine. Wanaeleza kuwa hali hii huwapo kwa sababu kuna sifa fulani za kufanana katika vitajwa viwili. Pia, Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa katika kamusi polisemia huonyeshwa kama neno moja lenye maana mbalimbali.

Hali kadhalika, Ullmann (1967) anaeleza kuwa polisemia ni sifa ya msingi katika mazungumzo ya binadamu ambapo licha ya kuwa na maana zaidi ya moja maana hizo zina uhusiano. Pia, anaeleza kuwa kwa kiasi kikubwa polisemia hutokana na uhamishaji wa matumizi ya neno hilo lakini hutegemeana na lugha inayohusika. Maelezo haya yanadokeza kuwa kuna uelekeo fulani wa maana katika polisemia ambao husababisha dhana ya mabadiliko ya maana kujidhihirisha waziwazi. Hivyo, makala hii inabainisha uelekeo wa maana za kipolisemia katika lugha ya Kiswahili. Lengo hasa likiwa ni kueleza utokeaji wake na namna zinavyoba- inishwa katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu na changamoto zinazoweza kujitokeza katika ubainishaji huo. Data iliyotumika ni kutoka katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 2013). Makala hii imeanza kwa kuelezea utangulizi. Halafu imefuatiwa na ufafanuzi wa nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data. Baada ya hapo tumeelezea dhana ya uelekeo wa maana katika polisemia. Pia tumefafanua uelekeo wa mabadiliko ya maana katika polisemia. Hali kadhalika, tumeelezea changamoto zinazojitokeza katika ujibainishaji wa polisemia katika kamusi. Mwisho kabisa ni hitimisho kwa ujumla.

## 2.0 Nadharia

Nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data ya makala hii ni ya Maana kama Dhana. Nadharia hii inahusu maana ya umbo la kiisimu kuwa ni mawazo au dhana zinazowianishwa katika akili ya mtu yeyote anayezielewa dhana hizo na vitu vinavyowakilishwa na maelezo hayo (Lyons, 1981). Hivyo, nadharia hii inadai kuwa, maana ni alama/picha ya mawazo iliyomo akilini mwa mzungumzaji. Ullmann (1964:57) anaeleza kuwa uhusiano wa neno na dhana ni wa makubaliano ya uwili, yaani mtu akitaka kusema neno hufikiria dhana au wazo fulani linalowianishwa na neno analotaka kusema. Vilevile, msikilizaji naye anapolisikia neno hulifikiria na kupata dhana fulani inayowianishwa na neno hilo. Hivyo, lazima pawe na makubaliano kati ya neno na dhana; na hiyo ndiyo maana. Ullmann (1964) anaeleza kuwa maana kwa mtazamo huu imejadiliwa na wanasemantiki miaka kama 30 iliyopita. Maana ya maneno huhusishwa moja kwa moja na wazo au taswira iliyopo akilini mwa mtu. Hii inatokana na kuwapo kwa maana za kimantiki (msingi) yaani dhana zinazoibuliwa na watumiaji wa lugha inayohusika, ambayo haihusishwi na muktadha wowote ule wa matumizi. Nadharia hii inatusaidia kuchunguza maana ya msingi (dhana) ambayo inahusiana na maana tofauti tofauti zilizojitokeza katika neno husika kutokana na mabadiliko ya maana, na hivyo kutuwezesha kubaini uelekeo wa maana katika utokeaji wa polisemia.

## 3.0 Dhana ya Uelekeo wa Maana katika Polisemia

Tunapozungumzia uelekeo wa maana katika polisemia tunamaanisha mabadiliko ya maana yanayojitokeza katika lugha na kusababisha utokeaji wa polisemia. Mabadiliko ya maana katika polisemia huhusu kuongezeka kwa maana katika mfumo wa kisemantiki huku umbo la neno likibaki vile vile (Kibiki, 2012). Hii inadhihirika umbo la neno linapobaki lilivyo lakini maana hupanuka zaidi.

Hivyo, basi neno likipanuka au likiongezeka maana husababisha uhusiano wa kifahiwa kama vile polisemia kwa sababu kunakuwa na uhusiano baina ya maana ya msingi na maana iliyoongezeka. Hii hudhihirisha uelekeo wa maana katika polisemia kuwa ni matokeo ya mabadiliko ya kisemantiki katika lugha husika.

### 3.1.1 Uelekeo wa Mabadiliko ya Maana katika Polisemia

Utokeaji wa polisemia sio maumbo tu ya kiisimu yanaanza moja kwa moja kuwa polisemia bali hujitokeza katika maendeleo ya kihistoria ambapo maana za ziada huibuka lakini bado huwa na maana ya msingi ya umbo hilo la kiisimu. Kwa hiyo, polisemia ni matokeo ya mchakato wa mabadiliko ya maana ambapo husababisha maana nyingine mpya zaidi ya ile maana ya msingi, hivyo kuongezeka kwa maana. Hivyo basi, matokeo ya mabadiliko ya maana ni muhimu katika utokeaji wa polisemia.

Aidha, polisemia ni uhusiano ambapo kuna umbo moja la neno lenye maana mbalimbali. Hivyo polisemia ni mahusiano ya maana ambapo maumbo ya lugha yanakuwa na maana zaidi ya moja lakini maana hizo zinakuwa na uhusiano. Maana za maneno hayo huwa zimepanuka kadri ya mpito wa wakati. Hali hii huwapo kwa sababu kuna sifa fulani za kufanana katika vitajwa viwili. Katika polisemia maana ya msingi ya neno hudokeza maana nyingine ya umbo. Kwa mfano, kuna uhusiano kati ya maana ya *mdomo wa chupa* na *mdomo wa binadamu*. Kwa sababu ya kuhusiana huku, neno linalotumiwa na kitajwa fulani *mdomo wa binadamu* huanza kutumiwa na kitajwa kingine *mdomo wa chupa*. Hapa “mdomo” ni mahali pa kuingizia kitu kama chakula na maji.

Mabadiliko ya maana katika polisemia hayatokei katika ombwe tu bali kuna uzi unaounganisha maana ya msingi na maana zinazoongezeka. Hivyo, maana mpya inakuwa na uhusiano wa kimaana na ile maana ya msingi. Uelekeo wa maana katika polisemia unadhihirisha kuwa mabadiliko ya maana za maneno hayaruki viunzi (maumbile hayaruki viunzi). Ni kweli tabia ya mabadiliko ya maneno hayaruki viunzi kwani kuna utaratibu fulani ambapo neno likibadilika maana yake lazima litakuwa na uhusiano na maana ile ya kwanza. Maana mpya zitakazobuniwa lazima zitahusiana na maana za msingi. Wazo hili linaungwa mkono na wataalamu kadhaa kama vile Katamba (1996), Growley (1998), Campbell (2004) na Kibiki (2012). Hivyo katika polisemia kupanuka kwa maana huhusisha uwezo wa neno kupata maana nyingi za ziada zaidi ya ile ya msingi, huku neno hilo likiendelea kutunza maana yake ya msingi, yaani haiwezi kupotea katika sehemu ya neno hilo. Aidha,

neno linaweza kupata maana nyinginezo za ziada huku likiendelea kutunza maana yake ya msingi (taz. Kibiki, 2012).

Jambo la muhimu katika kutambua maana mpya, yaani iliyoongezeka, ni muktadha kwa sababu maana ya msingi huwa moja katika miktadha yote lakini maana iliyoongezeka hujikita katika muktadha fulani. Hivyo, utokeaji wa polisemia huonekana kwa kujidhihirisha katika miktadha mipya. Uibukaji wa miktadha ndio unaisaidia kubaini maana mpya inayojitokeza. Hivyo miktadha tofauti tofauti ni vichocheo vya mabadiliko. Suala la muktadha limeongelewa pia na Narrog (2012) alipokuwa anaelezea kuhusu mabadiliko ya kisitiari kuwa huathiriwa na miktadha tofauti tofauti na kusababisha tofauti fulani za kisemantiki.

Katika polisemia maana huunganishwa na fikra moja. Neno moja huwa na maana zaidi ya moja kuelezea fikra/wazo moja. Kwa mfano, Kichwa - kichwa cha mtu, cha habari, cha ng`ombe, cha treni, cha chupa, n.k. Licha ya maana hizi kutofautiana lakini maana ya msingi hubaki palepale. Yapo mambo kadhaa yanayoweza kusababisha uibukaji wa polisemia, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya neno hilo. Yule (1985) anaeleza kuwa kupanuka kwa maana kunaweza kusababishwa na kuongezeka kwa matumizi ya neno hilo. Hivyo, wanajamii huanza kulitumia neno katika muktadha tofauti na kusababisha mabadiliko ya maana kuweza kutokea. Hali kadhalika Ullman (1962) na Massamba (1988) wanaeleza kuwa hisia za binadamu husababisha kuhusisha au kuhamisha maana ya kitu kimoja kupeleka katika kitu kingine. Hapo hujitokeza polisemia za kisitiari. Pia sababu nyingine ni analojia, hii hujitokeza kutokana na hali ya tabia ya kitu kufuata mkondo, au sura ya kitu kingine kilichotangulia (Sterm, 1931; Massamba, 1988). Massamba anatoa mfano na neno *mkuu* likiwa na maana ya mtu mwenye umri mkubwa lakini siku hizi ni mtu mwenye madaraka, uwezo au mtu aliyekabidhiwa dhima fulani.

Katika kamusi, neno lenye maana zaidi ya moja zinazohusiana huingizwa kama kidahizo kimoja kisha orodha ya maana za neno hilo huorodheshwa upande wa kulia kwa namba ikianza maana ya msingi, ambayo hutegemea uhalisia wake katika neno hilo. Kwa mfano, kama nomino asili yake ni binadamu (itaanza maana inayohusu binadamu), kama nomino asili yake ni kitu dhahiri na maana yake ya msingi itaanza hivyohivyo. Ikiwa ni kitenzi basi maana yake itaanza na tendo hilo husika, kama ni kivumishi maana yake huanza na sifa husika. Baada ya maana hii ya msingi maana nyingine hufuatia. Hivyo, uelekeo wa maana katika polisemia hujidhihirisha katika kamusi. Kwa mfano, maana ile ya msingi ndio huanza kuoneshwa ambayo mara nyingi huhusu binadamu au kitu dhahiri ndipo huweza kuanza kutokea maana nyingine za ziada. Hivyo, kamusi hutusaidia kubaini namna

polisemia zinavyoweza kujitokeza katika njia mbalimbali. Njia hizo ni kama zifuatazo:

Mosi, uhamishaji wa matumizi. Hapa hutokea neno moja linapokuwa na maana tofauti tofauti kutegemea na muktadha wa matumizi. Maana nyingine zinaibuka tu kwa muda mfupi lakini nyingine zinakuwa za muda mrefu na hatimaye hudumu na huweza kuingizwa katika kamusi. Kwa mfano, tazama mifano 1(a) – (e) hapa chini:

1 (a) **Mjinga** nm **1** mtu asiyejua kitu au jambo fulani; fala, jura. **2** tamko la dharau au tusi kwa anayechukuliwa kutojua kitu.

(b) **Mfinyanzi** nm **1** mtu anayefanya kazi ya kutengeneza vyombo vya udongo k.v vyungu. **2** udongo unaotumika kutengenezea vyungu.

(c) **Mdundo** nm **1** tendo la kugonga kwa vitu k.v ngoma. **2** upigaji wa kitu mahali pagumu ili kirudi au kipae juu. **3** mtwango wa kitu k.v kinu. **4** wimbo au muziki.

(d) **Mea** kt **1** chipuka kwa kitu kilichopandwa ardhini. **2** tokeza au kua kitu kwenye mwili wa binadamu, mnyama au mdudu: ~ nywele.

(e) **Gubiko** nm **1**. kitu cha kufunikia; mfuniko. **2** hali ya kufunikwa kabisa. **3** jambo lililofichwa; jambo la siri.

Tukichunguza kwa makini mifano hiyo tunaweza kubaini kuwa maana ya msingi ya maneno hayo ni ile inayopatikana katika namba moja kwa kila neno. Hivyo kutokana na wanadamu namna wanavyoitumia lugha yao katika kuumega ulimwengu wao kwa kutumia lugha ndipo huanza kutumia neno hilo katika mazingira mengine. Hivyo mwisho wake husababisha neno hilo kupata maana mpya tofauti na ile ya awali lakini zenye mahusiano fulani. Mifano hiyo 1 (a) – (e) inadhihirisha kwa uwazi kabisa kuwa imesababisha mabadiliko hayo ya maana kutokana na kuhamisha matumizi ya maana katika maneno hayo.

Ukiangalia mifano hiyo utaona kuwa maana ya msingi hutegemea uhalisi wa maana katika neno hilo, yaani maana ya msingi inaweza kuhusu mtu, kitu au hata tendo (inategemea maana ya asili ya neno hilo na aina ya neno hilo). Kwa mfano, katika 1 (a) na (b) maneno hayo ni nomino na maana ya msingi huanza na binadamu

mwenyewe anayetenda hayo, halafu neno hilo linatumika katika jambo lenyewe linalotendwa kama vile tamko au kitu. Kwa mfano, mfano 1(a) unaonesha kuwa maana ya msingi ni ile inayomhusu binadamu mwenyewe ambaye ana sifa hiyo, halafu inaanza kutumika kuonesha kuwa ni tamko linaloashiria tusi au kutokujua jambo fulani. Pamoja na hayo, maana hizi zote zina uhusiano na dhana ya kutokujua.

Hata hivyo, wakati mwingine huanza na kitu halisi ambayo ndio maana yake halisi, halafu huhamishiwa katika hali au jambo fulani kama tulivyoona katika mfano wa 1(e). Hii ni nomino ambayo imeanza na maana ya kitu chenyewe ambacho ni *mfuniko*, halafu maana ya hali yenyewe ya kufunikwa, kisha maana ikahamishiwa katika jambo linaloweza kufichwa. Hata hivyo, maana hizo zote zina uhusiano katika dhana ya kufunikwa. Pia, maana ya msingi huweza kuanza na matendo halisi; kwa mfano, katika 1(c) na (d) ambavyo ni vitenzi (matendo haya mara nyingi huhusisha binadamu na mazingira yake). Kutokana na matendo husika husababisha kutumia maneno hayo kuhamisha maana yake katika vitu vingine au hata dhana zingine kama vile za kidhahania na hatimaye husababisha kutumika katika jamii husika ili kukidhi lengo la mawasiliano.

Vilevile polisemia huibuka kutokana na neno moja kutumika katika uwanja mwingine maalumu ili kukidhi maana husika katika uwanja huo. Kwa mfano, uwanja huo unaweza kuwa wa kibiashara, kidini, kitaaluma, shughuli za kiserikali na kadhalika, kama ambavyo mfano 2 (a) – (c) unavyoonesha hapo chini:

2 (a) **Mtukufu** nm **1** sifa mojawapo ya Mwenyezi Mungu: aliyetukuka. **2** neno linalotangulia jina la mtu anayeheshimiwa (kar). ~ Rais.

(b) **Mkondo** nm **1** njia ya maji k.v. katika bahari. **2** njia isiyo ya kawaida inayofanywa na mtu au mnyama katika nyasi. **3** mchepuo kama vile madarasa. **4**. Njia ya mawimbi ya umeme au sauti inayowezesha kuvisafirisha vitu hivyo mpaka pale vinapohitajika.

(c) **Kidato** nm **1** mkato wa kupandia mnazi. **2** kipandio au kibao cha kupandia. **3** darasa katika shule za sekondari.

Ukichunguza kwa makini mifano hiyo 2 (a) – (c) utabaini kuwa maana hizo mpya zimetokana na maana ile ya kwanza ambayo ndiyo maana ya msingi. Maana hizo mpya nyingine zinatumika katika uwanja maalum kutokana na uhitaji wa kuhusisha maana hiyo katika muktadha mpya wa uwanja huo. Kwa mfano, mfano 1(a) unaonesha kuwa maana mpya imetokana na kutumia neno hilo katika uwanja rasmi kama vile serikalini kudhihirisha kiongozi aliyetukuka sana, mwenye hadhi ya juu na heshima kubwa kutokana na mamlaka aliyonayo kama vile *Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania*. Pamoja na hayo, maana hizi zina uhusiano na dhana ya kutukuka.

Hali kadhalika, katika mfano 1(b) na (c) inadhihirisha kuwa maneno hayo yamepata maana mpya baada ya kutumika katika uwanja wa elimu katika shule. Kwa mfano, katika 1(b) maana ya msingi ilikuwa ni njia ya maji, lakini imeweza kutumika kuonesha mchepuo wa darasa ambapo kuna uhusiano wa maana ya uelekeo mmoja unaoelekeana (njia fulani ya kuelekea pamoja). Katika mfano 1(c) maana ya msingi ilikuwa mkato wa kupandia mnazi yaani inatumika kukwea juu ya mnazi lakini neno hili pia limepewa maana ya darasa la shule ya sekondari. Hapa uhusiano wa maana upo katika dhana ya kupanda hatua kwenda juu zaidi.

Tatu ni lugha ya kisitiari ambapo utokeaji huu hutokana na mshikamano wa ufanano unaojidhihirisha katika sitiari. Kwa hiyo, uzi uunganishao baina ya maana ya msingi na mpya ni msingi wa ufananisho. Maana mpya inayojitokeza huwa ni sifa za ziada. Hivyo baada ya kuwapo na mfanano huo wa sifa hizo au tabia kati ya kitu kinachozungumziwa kwanza na kile kinachorejelea maana mpya ndipo husababisha uhamishaji wa sifa hizo au tabia. Mfano wa 3 hapo chini unaonesha namna polisemia za kisitiari zinavyojitokeza. Mara nyingi hutumiwa sifa alizonazo kiumbe hisivu kama vile binadamu, mnyama au mdudu. Sifa hizo huhamishiwa katika vitu vingine. Kwa mfano, tazama mifano 3(a) - (c) ifuatayo:

3 (a) **Kupe** nm **1** mdudu mdogo ambaye huganda kwenye miili ya wanyama na kuwafyonza damu. **2** mtu anayepata mapato bila ya kutumia jasho lake, mtu mwenye nguvu asiyefanya kazi bali hutegemea wengine.

(b) **Mguu** nm **1** kiungo cha mwili wa binadamu, mnyama au mdudu kinachomwezesha kusimama au kwenda. **2** kitu chochote kinachofanya kazi kama hiyo: ~ wa meza.

(c) **Mkono** nm **1** kiungo cha mtu kinachotokeza kwenye bega kinachotumiwa kushikia vitu. **2** kitu chochote kinachofanana na au kufanya kazi ya kushika vitu. **3** sehemu ndogo ya kitu inayojiunga au kutoka kwenye kitu hicho.

Ukichunguza kwa makini mifano 3 (a) – (c) utabaini waziwazi kuwa utokeaji wa sitiari ni njia mojawapo inayopelekea kupata polisemia katika lugha ya Kiswahili. Ukimakinikia maana hizo mpya utabaini kuwa zina uhusiano na maana ya msingi ambayo ipo katika namba moja kwa kila neno. Kwa mfano, katika 3 (b) na (c), utokeaji wake umebainika wazi ambapo binadamu anatumia sifa zinazotokana na maana ya viungo vyake vya mwili na kuhamishia sifa hizo katika vitu vingine na kusababisha kuibuka kwa maana mpya lakini yenye uhusiano na maana ile ya msingi. Katika mfano 3(b) maana ya msingi ya mguu wa binadamu pia huhusishwa katika vitu vingine vyenye uwezo wa kutenda kama mguu huo yaani kushikilia kiwiliwili, dhana hiyo ndiyo inayofanya kuwe na uhusiano. Kwa mfano, ukihusisha *mguu wa mtu* na *mguu wa meza*. Hata katika mfano 3(c) maana ya msingi ya neno mkono inahusishwa na maana hizo zaidi kutokana na uhusiano wa dhana ya kuweza kutenda kama vile mkono wa binadamu katika kushikilia. Lakini katika mfano wa 3(a) maana ya msingi itokanayo na tabia ya kupe mdudu kunyonya damu ili aendelee kuishi, huhamishiwa kwa binadamu ambaye anapata mapato bila ya kutumia jasho lake. Japokuwa kuna wakati upo uwezekano wa polisemia za kisitiari kuhusisha vitu vingine au dhana nyingine, mara nyingi zinahusu tabia au sifa za ziada za viumbe hisivu kama vile binadamu, wanyama na wadudu.

Nne, polisemia huibuka kutokana na dhana za kigeni. Ullman (1977) anaeleza kuwa hii ni njia mojawapo ambapo lugha inaweza ikachangiwa maana mpya kwa kubadilisha kiasi fulani maana ya ulimwengu uliopo. Hivyo wakati mwingine ukopaji unaongeza maana mpya katika neno ambalo tayari lipo katika lugha husika ili kupata dhana hiyo mpya ambayo kwa namna moja au nyingine awali ilikuwa haielezwi kwa uhalisi wake. Pia maana hiyo mpya bado inakuwa na uhusiano na maana ya msingi ya neno hilo. Tazama mfano 4 (a) – (c) unavyoonesha hapa chini:

4. (a) **Kufuru** kt **1** sema jambo ambalo ni kinyume na imani ya dini. **2** kataa kufuata imani ya dini baada ya kujua. (Kar)

   (b) **Boriti** nm 1 mti mrefu mnene utumiwao kujenga dari la nyumba. 2 mlingoti mrefu wa chuma, mhimili wa chuma cha pua. 3 aina ya nguo yenye michoro ya mistari iliyoelekezwa upande mmoja. (Kre)

   (c) **Programu** nm **1** mpango wa mambo ambayo mtu au kampuni inakusudia kuyafanya. **2** Mfumo wa kompyuta ulioandaliwa kwa ajili ya kutenda kazi fulani k.v kuandaa bili, kutengeneza vitabu au kupeleka na kupokea barua-pepe. (Kng)

Ukichunguza kwa makini mfano 4 (a) - (b) utabaini wazi kabisa maana hiyo mpya iliyojitokeza katika maneno hayo imetokana na utamaduni wa kigeni ambao ni Kiarabu, lakini mfano 4 (c) maana hiyo mpya imetokana na utamaduni wa kigeni ambao ni Kiingereza. Hivyo baada ya jamii ya Waswahili kuanza kuyatumia yakimaanisha maana hizo kutokana na utamaduni huo wa kigeni, tayari imesababisha kutokea kwa maana mpya ambayo ina uhusiano na maana ya msingi. Hivyo hayo ni mabadiliko ya maana kihistoria katika lugha husika. Hii ina maana kuwa maana ya msingi ya maneno hayo ilikuwapo kabla ya utamaduni wa kigeni lakini maana za ziada za maneno hayo hazikuwapo kabla ya utamaduni wa kigeni husika

Kwa mfano 4 (a) ni kitenzi ambapo maana yake ya msingi ilikuwa ni kusema jambo lolote ambalo lipo kinyume na imani ya dini yoyote ile pasipo kufungamana na utamaduni wa kigeni, lakini neno hili kutokana na dhana ya kigeni kutokana na Kiarabu linatumika pia pale ambapo unaamua kukataa kufuata imani ya dini wakati tayari umeshaijua. Hivyo, kuna tofauti fulani na maana ya msingi ya neno hilo. Lakini maana hizo zina uhusiano yaani zote zina dhana ya kuwa kinyume na masuala ya imani. Hali kadhalika, katika mfano 4 (b) maana ya msingi ya neno boriti ni mti mrefu utumiwao kujenga dari la nyumba lakini neno hili kutokana na dhana ya kigeni kutokana na Kireno linatumika kumaanisha mlingoti mrefu wa chuma, mhimili wa chuma cha pua. Pia humaanisha aina ya nguo yenye michoro ya mistari iliyoelekezwa upande mmoja. Hatahivyo licha ya maana hizo kutofautiana na maana ya msingi ya neno hilo lakini maana hizo zina uhusiano. Pia, katika mfano 4 (c)

maana ya msingi ya neno hilo kama mpango fulani, lakini maana mpya imetokana na utamaduni wa kigeni ambapo inaamaanisha mfumo huo kutokana na maendeleo ya teknolojia. Lakini maana hizo zina uhusiano katika dhana ya mambo yanayofanyika kwa utaratibu fulani.

Aidha, polisemia zinazoibuka kutokana na dhana za kigeni hujidhihirisha kwa uwazi pale ambapo dhana hiyo mpya hubainishwa kutokana na dhana za kigeni. Hii husaidia kupata dhana hiyo mpya ambayo hapo awali ilikuwa haielezwi katika dhana za kigeni.

Hivyo njia hizi zinazosababisha utokeaji wa polisemia zimesaidia kuonesha uelekeo wa maana katika polisemia ukoje. Hivyo katika njia hizo tulizozichunguza tumebaini kuwa njia ya kuhamisha matumizi, uwanja maalumu na lugha ya kisitiari, ndizo hutumika sana katika kuleta mabadiliko ya maana katika maisha ya kila siku na kusababisha kuzidi kuongezeka kwa polisemia katika lugha. Hali kadhalika, njia ya ukopaji kutoka katika lugha nyingine nayo inatumika na kusababisha kuongezeka kwa polisemia katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kuna utofauti fulani miongoni mwa njia hizo kama tulivyoona katika kila kipengele.

## 4.0 Changamoto

Katika uingizaji wa polisemia katika kamusi, kuna wakati mwingine husababisha mkanganyiko baina ya polisemia na homonimia[1]. Hii hutokana na polisemia kuhusiana na neno moja kuwa na maana zaidi ya moja. Hata hivyo angalizo kubwa ili kuweza kuepuka mkanganyiko huo ni kuwa katika polisemia maana hizo huwa zinakuwa na uhusiano lakini katika homonimia maana hizo huwa hazina uhusiano wowote ule. Kwa mfano, neno kichwa katika kamusi limeingizwa kama homonimia badala ya polisemia. Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* Toleo la Tatu (TUKI, 2013) imeingizwa kama ifuatavyo:

---

[1] Homonimia ni leksimu mbili au zaidi katika lugha moja zenye kuandikwa sawa lakini zenye maana tofauti (taz. TUKI, 2009:30).

**Kichwa** *nm* sehemu ya mwili wa mnyama au binadamu iliyoshikana na shingo na ambayo ina ubongo, mdomo, pua, macho, masikio na nywele.

**Kichwa** *nm* injini ya garimoshi ambayo hukokotoa mabehewa. ~ cha garimoshi.

**Kichwa** *nm* maneno machache yaliyoandikwa juu ya habari au taarifa: ~ cha habari.

**Kichwa** *nm* mtu anayeongoza shughuli fulani katika familia au jamii; kiongozi.

Mifano hii inaonesha wazi uhusiano wa maana hizo na maana ya msingi licha ya kutumika katika miktadha tofauti tofauti. Hivyo uchunguzi wa kina unahitajika katika maneno kama haya ili kuweza kuepuka mkanganyiko huo.

## 5.0 Hitimisho

Matokeo katika makala hii yameonyesha kuwa polisemia huwa na maana zaidi ya moja zinazohusishwa na fikra/wazo moja (maana ya msingi), utokeaji wake upo wa aina tofauti; ambao ni uhamishaji wa matumizi, ufananisho wa kisitiari, uwanja maalum katika jamii na hata kuwapo kwa maneno yenye asili ya kigeni. Vilevile, wakati mwingine utokeaji huu hutegemeana na aina ya neno husika kama vile nomino au kitenzi. Hali hii hujibainisha wazi katika kamusi. Kwa mfano, kama ni nomino maana ya msingi huweza kuanza na mtu, mnyama au mdudu au kitu halafu ndipo jambo fulani au dhana dhahania hufuatia. Kama ni kitenzi maana ya msingi huanza na matendo yenyewe kisha ndipo ijidhihirishe katika vitu vingine au hata kwa binadamu. Lakini hali hii hutegemea maana ya asili ya neno hilo na utokeaji wake.

Hata hivyo, kuna baadhi ya polisemia huwa na changamoto katika namna zilivyobainishwa katika kamusi. Kwa mfano; neno **kichwa** limeingizwa kama maneno manne tofauti likimaanisha homonimia lakini ukichunguza maneno hayo yote yana uhusiano na maana ya msingi. Hivyo kuna uhitaji wa kuelewa uelekeo wa

maana katika polisemia ili kuepusha mkanganyiko kwa watumiaji wa lugha husika. Hata hivyo, utokeaji wa polisemia umetudhihirishia dhana ya uwekevu katika lugha, yaani binadamu anapenda kurahisisha matumizi ya lugha. Hivyo kuwapo kwa umbo moja lenye maana tofauti inamaanisha uwekevu katika lugha yaani kuepuka kuwa na maumbo mengi katika lugha bila sababu maalum. Pia, kuwapo kwa umbo moja husababisha msamiati wa lugha fulani kutokaa holela bali kuwa na mfungamano fulani wa kimaana.

## Marejeleo

Campbell, L. (2004). *Historical Linguistics: An Introduction.* Edinburgh: Edinburg University Press.

Crowley, T. (1998). *An Introduction to Historical Linguistics*. Oxford: Oxford University Press.

Habwe, H. J. na Karanja P. K. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Katamba na Wenzake. (1996). *Contemporary Linguistics: An Introduction*. London: Clark Pitman Ltd.

Kibiki, J. M. (2012). *Mabadiliko ya Maana katika Vitenzi vya Kiswahili*. Tasinifu ya M.A Kiswahili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lyons, J. (1981). *Language Meaning and Context.* London: Cambridge University Press.

Massamba, D.P.B. (1988). "Sababu za kubadilika kwa maana za maneno: Mifano kutoka Kiswahili" Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (juzuu no: 55).

Narrog, H. (2012). *Modality, Subjectivity and Semantic Change: A Linguistic Perspective*. New York: Oxford University Press.

Sterm, G. (1931). *Meaning and Change of Meaning with special reference to the English Language*. Bloomington: Indian University Press

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

Ullmann, S. (1962). Semantics: *An Introduction to The Science of Meaning*. Oxford: Basili Blackwell.

______(1964). *Semantics: An Introduction to the Science of meaning.* New York: Oxford Basil Blackwell.

______(1977). *Semantics An Introduction to The Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell.

Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press.